Uongozi na Utawala wa Shule

Jamii ya kujifunza ya Walimu Wakuu

(Kujifunza pamoja na wengine)

Kitabu hiki ni mwongozo wa kuunda Jamii ya kujifunza ya Walimu Wakuu

Yaliyomo

SURA YA KWANZA 3
UTANGULIZI 3
1.1 Jamii ya kujifunza ya Walimu Wakuu ni nini? 3
1.2 Kusudi la jamii ya kujifunza ya Ya Ya Walimu Wakuu: 3
1.3 Namna ya kufanya jamii ya kujifunza ifanye kazi 3
SURA YA PILI 4
MCHAKATO WA KUUNDA JAMII YA KUJIFUNZA YA WALIMU 4
2.1 Kuunda ushirika 4
2.2 Kutafuta kusudi la pamoja 5
2.3 Kutafuta njia ya kufikia mabadiliko 5
2.4 Kutafuta ujuzi/maarifa/uzoefu tulionao kama jamii ya kujifunza 6
2.5 Maelezo ya jumla ya kazi za jamii yetu ya kujifunza 8
SURA YA TATU 9
ZANA NA MBINU ZINAZOMSAIDIA MWANAJAMII YA KUJIFUNZA KUWA MAHIRI 9
3.1 Ngazi ya tafsiri 9
3.2 Jinsi ya kufanya mambo yaende vizuri unapokutana na ukinzani 11
3.3 Tambua vikwazo vinavyotoka ndani yako 11
3.4 Majadiliano; maana, kanuni, utaratibu 13

SURA YA KWANZA

Utangulizi

1.1 Jamii ya kujifunza ya Walimu Wakuu ni nini?

Jamii ya ujifunzaji ya Walimu Wakuu ni kikundi cha Walimu Wakuu waliotengeneza ushirika, wenye hamu, kusudi, malengo na mtazamo unaofanana, wanaokutana mara kwa mara ili kubadilishana uzoefu na kujifunza kwa ajili ya maendeleo ya shule zao.

1.2 Kusudi la jamii ya kujifunza ya Walimu Wakuu:

- Kushirikishana uzoefu, ujuzi, maarifa, hofu na mashaka
- Kusaidia ya Walimu Wakuu kujifunza mambo mazuri kutoka kwa kila mmoja
- Kusaidia Walimu Wakuu kuwa na ufanisi katika kutekeleza mabadiliko
- Kuboresha utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya shule

1.3 Namna ya kufanya jamii ya kujifunza ifanye kazi

Kila wakati unapopata ugumu wa jambo fulani, tumia zana na mbinu zilizowekwa kwenye sura ya 3:

- Jaza ngazi ya tafsiri (Kama umepata mazingira yaliyokusababishia jazba)
- Fanyia kazi hatua za kukabiliana na ukinzani (kutoka kwa wafanyakazi, wazazi) na andika majibu ya maswali na weka kumbukumbu
- Jaza karatasi ili kubaini vikwazo vinavyotoka ndani yako (pale inapotokea mawazo/mabadiliko yanapoonekana kushindwa kufanya kazi kutokana na mitazamo yako)

Waombe wanajamii ya kujifunza wenzako wakusaidie kuchunguza/kudadisi na kulielewa tatizo lako. Utakuwa umeshajaza maelezo juu ya tatizo lako kwenye karatasi ya mazoezi na utawaomba wenzako wafanye majadiliano na wewe. Watakuuliza maswali ya kiuchunguzi/ udadisi ambayo yatakusaidia kwenye mambo yafuatayo:

- Kuelewa hatua zako zisizo na ufanisi
- Kufanya mambo yaendelee hasa pale unapokutana na ukinzani
- Kubaini hofu na mawazo yanayozuia ufanisi wa mabadiliko unayotaka yatokee

SURA YA PILI

Mchakato wa kuunda jamii ya kujifunza ya Walimu

2.1 Kuunda ushirika

Unaweza kuunda ushirika na mwalimu mkuu mwingine yeyote. Lakini hakikisha kwamba ushirika wenu unatekelezeka kwa urahisi na ufanisi. Washiriki muweze kukutana mara kwa mara bila gharama kubwa (washirka watoke maeneo yaliyo karibu). Jaza jedwali hapo chini ili kutoa maoni yako juu ya kutekelezeka kwa ushirika unaotarajia kuunda:

Nitaunda ushirika huu wa jamii ya kujifunza ya Walimu Wakuu na nani?	**Nitampataje na wapi, Mwalimu Mkuu mwenzangu ninayeweza kushirikishana naye changamoto, hisia na hulka yangu?**	**Namna gani tutaanza jamii ya ujifunzaji?**	**Lini tutaaanza jamii ya ujifunzaji?**	**Tutafanya kazi na nani? Tutaunganishaje jamii yetu ya ujifunzaji na utekelezaji wa mpango wa maendeleo ya shule?**

Wanachama wa jamii yetu ya kujifunza ya Walimu Wakuu (wanachama 3 hadi 9):
• • • • • •

2.2 Kutafuta kusudi la pamoja

Unapokutana na wenzako kwa mara ya kwanza kama jamii ya ujifunzaji ya Walimu Wakuu, mtafanya majadiliano ili kubaini Imani na mitazamo mliyonayo kwa pamoja na wenzako. Maana ya majadiliano haya ni kuulizana maswali ya ufafanuzi, udadisi na kusikilizana kwa hisia za kuonja kile kinachozungumzwa.

Ndoto na matamanio yetu ya pamoja:

Kama mmeshabaini ndoto na matarajio ya pamoja kama kundi, endeleeni kutengeneza kusudi la pamoja, kitu mnachotaka kundi lenu lifikie kwa kufanya kazi pamoja.

Kusudi letu la pamoja (Lengo letu):

Kusudi la pamoja ni jambo linalowafanya kama jamii ya kujifunza mlifanyie kazi kwa pamoja, jambo linaloweza kuwaunganisha na kufanya jamii yenu iwe pamoja.

2.3 Kutafuta njia ya kufikia mabadiliko

Angalia kusudi la pamoja la kikundi chenu.

Fikiria kuhusu mabadiliko yaliyoletwa shuleni kwako (Mpango wa maendeleo ya shule, Ruzuku ya shule, Mkutano wa kila wiki wa walimu, mafunzo kwa walimu, mfumo wa taarifa za shule, mpango wa utayari, ubao wa matangazo, ushirikiano wa walimu na wazazi, n.k). Umetekelezaje hadi sasa? Kitu gani unahitaji kukifanyia kazi zaidi ili ufikie kusudi la pamoja la jamii yako ya ujifunzaji?

- Tuna uzoefu gani utakaosaidia kuboresha shule zetu? Tumejifunza nini?
- Nini kimefanywa na Walimu Wakuu wengine kilichosababisha mafanikio yao?
- Kwanini wamefanikiwa? Zipi ni sababu za mafanilkio yao?
- Nitaboreshaje hali iliyopo kwenye shule yangu?

- Kitu gani nimejaribu (Lakini bila mafanikio)?
- Nifanye nini tofauti ili nifanikiwe kuboresha mabadiliko?
- Mabadiliko yaliyoletwa yameboresha vipi ustawi na ubora wa ujifunzaji kwa wanafunzi?
- Tutatumiaje mazuri na mabaya tuliojifunza ili kufanikisha kusudi letu la pamoja?
- Naweza kujifunza nini kutoka kwenye jamii yangu ya kujifunza?

Vitu tunavyohitaji kufanyia maboresho (Hatua za kuchukua ili kufikia kusudi letu):

2.4 Kutafuta ujuzi/maarifa/uzoefu tulionao kama jamii ya kujifunza

Fikiria zana, mbinu, na ujuzi ulioupata kwenye MMS, mikutano ya kila wiki ya walimu, mfumo wa taarifa za shule, n.k (Stadi za kusikiliza na kuuliza maswali, stadi za kufanya mashauri na wadau, uchambuzi wa mti wa matatizo, stadi za mawasiliano, n.k). Jadili kitu ngani mnaweza kujifunza kutoka kwa kila mmoja wenu na kivipi mnaweza kujifunza. Mnapaswa kutumia zana na mbinu mlizopewa kwenye sura ya 3.

Mifano ya mbinu hizo ni kama:

- Kufanyia mazoezi stadi mpya
- Kuonesha utekelezaji wa stadi mpykwa vitendo na kujadili na wenzako iliendaje
- Kuitumia stadi mpya/ wazo jipya halafu kujadili na wengine juu ya uzoefu uliopatikana
- Kuchunguza/kuangalia utekelezaji wa wazo/stadi mpya, kutembelea shule nyingine
- Kuandaa mkutano wa wanajamii ya kujifunza ili kujadili hoja au wazo jipya
- Kufanya jaribio la utekelezaji wa wazo/jambo jipya

Uwezo wetu kama jamii ya kujifunza (Sisi tupo vizuri kwenye nini)**:**

Namna ya kutumia maarifa/ujuzi/uzoefu tulionao

Fanyia kazi mlolongo wa kimantiki wa Jamii ya kujifunza na uweke kwenye mzunguko kwa ajili ya kujifunza kwa ushirikiano:



Mtandao wetu wa kusaidiana

- Nani mshirika wetu?
- Ikitokea tunataka taarifa ambayo sisi kama kundi hatuna, tutafanya kazi na nani ili kupata taarifa hiyo (Afisa Elimu Kata, Ofisa Elimu wa Wilaya, Ofisa Elimu wa Mkoa, Mdhibiti Ubora wa Shule, au Kituo cha utayari)?
- Washirika wetu watachangiaje mafanikio ya lengo letu?

Washirika wetu:

2.5 Maelezo ya jumla ya kazi za jamii yetu ya kujifunza

Kutengeneza jalada la kumbukumbu za jamii ya kujifunza

Siku ya kuanza kwa jamii yetu ya kujifunza:	
Kusudi/lengo letu la pamoja:	
Njia yetu ya kufikia mabadiliko:	
Maarifa/Ujuzi/Uzoefu tulionao, mfumo wa kujifunza kwa ushirikiano, na mafanikio yetu:	
Shule 1	
Shule 2	
Shule 3	
Shule 4	
Shule 5	
Shule 6	
Shule 7	
Shule 8	
Shule 9	

1.

SURA YA TATU

Zana na mbinu zinazomsaidia mwanajamii ya kujifunza kuwa mahiri

3.1 Ngazi ya tafsiri

Unapojikuta upo kwenye mazingira/hali ngumu, ngazi ya tafsiri ni zana itakayo kusaidia kuelewa vizuri hatua ulizochukua (na itasaidia kuboresha hatua hizo kwa siku za badae).

Hatua 4. Maamuzi/Hatua Unachukua hatua gani?	
Hatua 3. Hitimisho Nini hitimisho lako?	
Hatua 2. Tafsiri Unaielezaje/umeielewaje sehemu ya taarifa iliyokuchochea? Ina maana gani kwako?	
Hatua 1. Uchaguzi Ni sehemu gani ya taarifa/tukio imevuta umakini wako? Ni sehemu gani ya taarifa imekuwa chochezi kwako?	

Namna ya kujaza ngazi ya tafsiri

Kama umefanya maamuzi au umechukua hatua ambazo zisizo na ufanisi, jaza ngazi ya tafsiri ili kuelewa vizuri hatua uliyoichukua. Anza kujaza ukianzia hatua ya 1 (kutoka chini). Usifikirie kuhusu majibu yako bali andika kile unachodhani kama ingetokea umepatwa na hali/mazingira hayo magumu:

Hatua ya 1. Andika kitu kilichovuta umakini wako au kilichokuchochea.

Hatua ya 2. Andika ulivyojisikia baada ya kuona kilichotokea. Huna haja ya kufikiria sana, eleza tafsiri yako tu juu ya kilichotokea au ulichokiona/ kilichokuchochea!

Hatua ya 3. Hatua hii inahusu hitimosho lako. Huwa tunafanya hitimisho kwa haraka sana. Huenda tayari umeshafanya hitimisho juu ya ulichokiona/Kichocheo. Andika hitimisho hilo!

Hatua ya 4. Ni Dhahiri unajua hatua gani ungechukua kutokana na ulichokiona/Kichocheo. Andika hatua hiyo, usifikirie, kuwa mkweli, hakuna hatua sahihi wala isiyo sahihi.

Namna ya kujenga uelewa kwa kutumia ngazi ya tafsiri

Ili kuelewa hatua zako ulizochukua zisizo na ufanisi, inakupasa kueleza tukio zima kwa kutumia tafsiri ya ngazi kwa mwanajamii ya kujifunza mwenzako:

- Jieleze kuhusu wewe mwenyewe (wengine wanaweza kuwa na tafsiri na hitimisho tofauti na lako). Mimi nimeona…, nadhani…, nimeelewa…, nimemaanisha…, imenifanya nijisikie…, nimeamua…
- Anza na hatua ya 1 (Sehemu ya taarifa iliyokuchochea) au hatua ya 4 (Maamuzi uliyoyafanya/Hatua uliyoichukua). Unaweza kuanza chini au juu
- Elezea hitimisho lako kama chaguo lako (Ni hitimisho lako tu na si ukweli usioepukika)
- Changia mifano mbali mbali na yale ya ukweli pia kwa mwanajamii ya kujifunza mwenzako
- Kila mmoja wenu ajaribu kuhakikisha kwamba anamuelewa mwenzake kwa kila hatua aliyoieleza
- Wape nafasi wenzako wakuulize maswali ya ufafanuzi, ili wakueleze kama kuna kitu umekiacha/ umekosea
- Wape nafasi wenzako wakuoneshe kama hoja yako si halali



- ***Ngazi ya tafsiri*** *ni zana ya kutujengea uelewa kati yetu kwasababu inatufanya tutambue kwamba sisi ni wote* :
  - Huwa tunachagua taarifa (Kichocheo)
  - Tunafanya tafsiri ya taarifa tulioichagua
  - Tunafanya hitimisho
  - Na mawazo na tafsiri hizi zinatupelekea kufanya maamuzi au kuchukua hatua!
- Kutoelewana baina yetu kunatokea kwasababu, kwa kutumia tukio moja **tunachagua kichocheo tofauti na kufanya tafsiri tofauti**, **tunafanya hitimisho tofauti**, na hatimaye **tunafanya maamuzi au tunachukua hatua tofauti!**

3.2 Jinsi ya kufanya mambo yaende vizuri unapokutana na ukinzani

Unapokutana na ukinzani, unaweza kutumia hatua nne za kwenye jedwali hapo chini na kuona kama mambo yanaweza kwenda vizuri tena. Andika majibu ya maswali na weka kumbukumbu ili uweze kuelezea tatizo lako kwenye kikao cha jamii yako ya kujifunza. Ukishawasilisha tatizo, wanakikundi wenzako watakuuliza maswali ya kudadisi (Majadiliano). Maswali hayo yatakusaidia kuwa na uelewa zaidi juu ya ulichokifanya na kwanini kimefanikiwa au hakijafanikiwa.

1. Tambua ukinzani	Kama mwalimu, mwanafunzi au mzazi anapingana na jambo, msikilize kwa makini. Halafu bainisha jambo anayodhani si halali, si ya haki, hayakubaliki. Ana hofu/ mashaka gani juu ya jambo hilo?
2. Dadisi (Uliza maswali)	Ili kuelewa wasi wasi/ hofu au ukinzani, uliza maswali ya ufafanuzi, kwa mfano: • Nini hasa kigumu kama ukitaka.....? • Kitu gani unakiona si sahihi au hakikubaliki? • Unaweza kutoa mfano wa kitu usichokuwa na uhakika nacho? • Huna uhakika kuhusu nini? • Unaweza kutoa mfano wa jambo unalodhani halitafanikiwa? • Unadhani halitafanikiwa kwa sababu gani? • Unaweza kuniambia ni kitu gani unaogopa?
3. Kukubali	Waambie wengine kwamba umeshaelewa jambo linalomfanya mwenzenu apate hofu/ wasi wasi. Usijadili kuhusu ukinzani, ila taja huo ukinzani.
4. Toa msaada	Mtu mwingine anaweza kuwa na mawazo ni kwa jinsi gani jambo linalokupa ugumu linaweza kuboreshwa na kuwa rahisi. Anaweza kuwa na uelewa mkubwa juu ya nini kinaweza kufanya kazi kwake. Muombe mtu huyo akujuze jinsi gani anadhani jambo hilo linaweza kufanyika vizuri na kwa urahisi, na wewe ujifunze kutokana na uzoefu wake. Kwa mfano : • Ungetatuaje ugumu wa jambo hili?

3.3 Tambua vikwazo vinavyotoka ndani yako

Shule yako inatekeleza shughuli mbali mbali zenye lengo la kuboresha elimu. Kuna baadhi ya shughuli hizo haziendi sawa kama ilivyotarajiwa na unataka kufahamu kwanini haziendi sawa. Umewaomba wenzako wakusaidie kubaini ni kwa namna gani unaweza kufanya shughuli hizo ziende sawa kama inavyotarajiwa.

Jiandae kulieleza tatizo/ jambo lako. Halafu jaza kwenye jedwali; kitu gani unakikubali/unakiamini, jambo gani hukubaliani nalo, au una wasiwasi nalo, na unadhani nini kingefanyika (lakini hujafanya)

Kuandika mawazo yako kwenye karatasi kutakusaidia kulieleza tatizo/jambo lako kwa wanajamii wenzako. Itakuwa ni rahisi kwa wanajamii wenzako kuuliza maswali ya ufafanuzi

Tatizo/ Jambo linalonisumbua:

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

_____

Na haya ndo mawazo yangu, na mwitikio wangu (kile ninachodhani, kile nilichosema)
Mawazo niliyoyakubali:
Kile nilichokuwa na hofu nacho, Kile nisichokikubali, au nilichokuwa na mashaka nacho (ila sijasema):
Kitu ambacho ningefanya, ila sikufanya kwasababu:

Mabadiliko ninayoyakubali:	**Kile nilichokihofia (lakini sijasema):**	**Jinsi imani na wasi wasi wangu ilivyozuia mabadiliko tarajiwa:**
Ubora wa ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi		

Mazingira salama ya kujifunzia kwa wanafunzi		
Maboreko ya ustawi kwa wanafunzi		

3.4 Majadiliano; maana, kanuni, utaratibu

Majadiliano ni nini?

- Majadiliano ni mazungumzo yaliyopangwa kwa kufuata utaratibu maalum. Majadiliano ni zana inayotumika kuelezea, kuchambua, kufafanua na kuunda wazo na tabia (maamuzi).
- Wakati wa majadiliano washiriki husikiliza mawazo ya kila mmoja na huulizana maswali ili kutafuta maana halisi iliyopo kwenye wazo linalojadiliwa

Kanuni muhimu za majadiliano:

- Majadiliano yanapaswa kufanywa taratibu, kuakisi wazo husika, kuvumbua, kufafanua na kuunda maana ya pamoja kwa washiriki.
- Kwenye majadiliano kusikiliza kuna haki sawa kama ilivyo kwa kuongea.
- Kundi zima lina wajibu wa kuhakikisha majadiliano yanaendeshwa ka utulivu.
- ***Majadiliano hayana matokeo mengine zaidi ya majadiliano yenyewe***! Majadiliano hayana maana ya kufikia hitimisho, ni kupanga na kufikia maelewano!

Utaratibu wa majadiliano:

1. Wasilisha kwenye jamii yenu jambo linalomsumbua mmoja wenu

2. Fanya uchambuzi na fafanua jambo linalosumbua

- Maana ya kufanya uchambuzi ni kuuliza maswali ya ufafanuzi ili kupata picha halisi ya jambo linalosumbua. Mfano wa maswali hayo ni kama:
  - Tatizo lilitokea lini?
  - Una maana gani unaposema.....?
  - Unaweza kutueleza nini zaidi kuhusu hilo?

- Kitu ambacho bado sijaelewa ni....
- Ulifanya nini, umefanya nini hasa?
- Tatizo lipoje hasa, kipi ni kigumu?
- Unaweza kujua ni kwanini hufanikiwi?

Usitoe mawazo yako, vikwazo au kutokubaliana!

3. Hisia, kuelewa na kuvaa viatu vya mwingine mwenye tatizo

Chukulia kwamba wewe ndiwe una tatizo linalomsibu mwalimu mkuu mwenzako. Fikiria ungejihisi vipi, ungefikiria nini, au ungefanya nini, au ungejaribu kufanya nini ili kukabiliana na tatizo, kwa wakati huo.

Shirikisha uelewa wako kuhusu changamoto kwa kuuliza maswali (kwa mfano):

- Umejisikia..... (Jaribu kufikiri ungekuwa na hisia gani, kwa mfano, nini kinakera, nini kina utata, kilichokukasirisha...)
- Ulidhani..... (Fikiria ni mawazo gani wengine wanaweza kuwa nayo)
- Uli..... (Sema kitu gani ungefanya)
- Ulijaribu..... (eleza jibu lako lingesaidiaje kukabiliana na tatizo)

4. Umuhimu wa kukabiliana na jambo linalosumbua

Nenda kwenye kiini cha tatizo. Jaribu kubaini msingi wa jambo linasumbua.

- Chunguza na jibu maswali kama:
  - Ni nini hasa?
  - Kipi kimegusa hisia zangu?
  - Kama ningepata nafasi ya kurudia, ningefanya nini cha utofauti?
  - Nimepata somo gani au nimejifunza nini?